

watoto Mitaa wa Jang'ombe Wilaya ya Mjini Unguja, jana. (Picha na Ikulu).

# \*Wizara ya Mifugo yazindua awamu ya pili 'Jenga Kesho'

Na MWANDISHI WETU

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu, imezindua awamu ya pili ya programu ya Jenga Kesho iliyo Bora kwa wanawake na vijana kwa sekta ya uvuvi "BBT-LIFE".

Tukio hilo lilitanyika juzi katika ofisi za Wakala ya Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kampasi ya Mbegani Bagamoyo mkoani Pwani.

Uzinduzi huo ambao umetanguliwa na mafunzo ya siku tano ya kubadili fikra kwa vijana na wanawake 300 waliochaguliwa kunufaika na awamu ya pili.

Programu hiyo ilifanywa na Naibu Katibu Mkuu

wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi), Agness Meena, ambaye aliwasisitiza vijana kuhakikisha wanatumia vema mafunzo kwa vitendo watakayopewa kwa muda wa miezi mitatu kwenye vituo walivypangiwa baada ya kukamilika kwa mafunzo hayo ya nadharia.

Agness aliongeza kuwa lengo la Wizara yake ni kutengeneza vijana na wanawake watakoakuwa wajasiriamali wakubwa kwenye upande wa sekta ya uvuvi kupitia ufugaji wa samaki katika vyanzo vya asili vya maji chumvi na baridi, mabwawa na kilimo cha zao la mwani.

Mkurugenzi Msaidizi-Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Robert Masingiri, alibainisha utekelezaji wa awamu ya pili ya programu ya

BBT-LIFE ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya Taifa ya kukuza ujuzi nchini kupitia kipengele cha mafunzo ya wanagenzi.

"Programu hii yote inagharamiwa na Serikali na kila mwaka huwa inatenga sh. bilioni tisa kwa ajili ya kuhakikisha vijana na wanawake wanapata ujuzi stahiki ili waveze kujajiri na mpaka sasa imeshatoa kiasi cha sh. bilioni 5.5 kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo" Alisema Masingiri.

Mwakilishi wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB), Kezilahabi Jumanne alisema walipata nafasi ya kutoa elimu ya uandaaji maandiko ya kibiashara kwa wanufaika hao hivyo anaamini baada ya kuhitimmo mafunzo hayo baadhi yao watakuwa wateja wao wa moja kwa moja kupitia mikopo watakayowawezesha.